**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. MAKAME MBARAWA (MB), WAZIRI WA MAJI AKIMUWAKILISHA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MARA MUGUMU, SERENGETI,**

**TAREHE 15 SEPTEMBA, 2019**

***Mhe. Adam Kighoma Malima - Mkuu wa Mkoa wa Mara,***

***Waheshimiwa Mawaziri kutoka Tanzania na Kenya,***

***Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Kaunti katika Ukanda wa Bonde la Mto Mara,***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya kutoka Tanzania na Kenya,***

***Waheshimiwa Wabunge kutoka katika Ukanda wa Bonde la Mto Mara,***

***Makatibu Wakuu wa Wizara kutoka Tanzania na Kenya,***

***Makatibu Tawala wa Mikoa iliyopo katika Ukanda wa Bonde la Mto Mara,***

***Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria,***

***Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya,***

***Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya,***

***Wataalamu kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali,***

***Wawakilishi kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali,***

***Washirika wa Maendeleo,***

***Wawakikishi kutoka Vyama vya Siasa,***

***Viongozi wa Dini,***

***Waandishi wa Habari,***

***Wageni Waalikwa,***

***Mabibi na Mabwana.***

## 1. UTANGULIZI

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kusafiri salama na kukutana hapa Mugumu, Wilaya ya Serengeti siku ya leo. Kama mnavyofahamu,

maadhimisho haya yalipaswa kufunguliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kutokana na kuwa na majukumu mengine imempendeza nimuwakilishe katika shughuli ya leo. Mheshimiwa Waziri Mkuu anashukuru sana kwa kumualika na anawatakia maadhimisho mazuri na yenye mafanikio.

Nichukue fursa hii kuwashukuru; Mkuu wa Mkoa wa Mara na waratibu wa masuala ya Bonde la Mto Mara na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kwa kushirikiana kuandaa maadhimisho haya. Kipekee niwashukuru Wananchi wa Wilaya ya Serengeti kwa mapokezi mazuri mliyotupa wageni wote.

Napenda pia kuwashukuru washiriki wote mlioweza kufika hapa Serengeti hususani wageni wetu kutoka Jamhuri ya Kenya. Mmeyapa maadhimisho haya umuhimu wa hali ya juu na ushiriki wetu ni uthibitisho tosha wa jinsi nchi zetu za Tanzania na Kenya zinavyoshirikiana katika utunzaji wa mazingira na rasilimali maji

katika Bonde la Mto Mara kwa mustakabali wa kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

## 2. SABABU ZA MAADHIMISHO YA SIKU YA MARA

**Ndugu washiriki;** Mto Mara unaanzia katika chemchem ya Enapuyapui iliyo kwenye misitu ya Milima ya Mau katika nchi ya Kenya ambapo maji ya Mto huo hutiririka kupitia pori la akiba la Hifadhi ya Taifa ya Maasai-Mara kwa upande wa Kenya na hatimaye katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA) kwa upande wa Tanzania, kabla ya kumwaga maji yake katika Ziwa Victoria. Mto huu unapita katika Wilaya nne kwa upande wa Tanzania ambazo ni Serengeti, Tarime, Rorya na Butiama.

Bonde la Mto Mara, ni moja kati ya mabonde yenye mito inayoingia katika Ziwa Victoria. Bonde hili linahusisha nchi mbili, yaani Tanzania (ambayo ina miliki asilimia 35 ya eneo la Bonde) na Kenya (inayomiliki asilimia 65 ya eneo lote la Bonde). Bonde la

Mto Mara ni eneo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi pamoja na baioanuai zilizopo.

Kwa kuzingatia umuhimu huu, Mkutano wa 10 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Bonde la Ziwa Victoria liliamua kuwe na Maadhimisho ya Siku ya Mara kila mwaka ifikapo tarehe 15 Septemba ili kuhamasisha na kutoa elimu kwa wadau juu ya utunzaji wa mazingira na rasilimali maji za Bonde la Mto huo.

**Ndugu Washiriki;** Kama mnavyofahamu, Maadhimisho hayo tangu mwaka 2012 hadi 2019 yamefanyika mara nane (8). Hadi sasa Kenya yamefanyika mara nne (4) na Tanzania mara nne (4); Maadhimisho ya saba (7) ya Mwaka 2018 yalifanyika Narok, Kenya tarehe 15 Septemba, 2018. Kenya kama mwenyeji wa maadhimisho hayo ilipokea wageni kutoka upande wa Tanzania na wadau mbalimbali wa maendeleo katika Bonde la Ziwa Victoria kuadhimisha Siku ya Mara. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Kenya kwa

kufanikisha sherehe hizo za mwaka jana.

Maadhimisho ya Nane (8) ya Siku ya Mara mwaka huu Kaulimbiu yake ni ***"Mimi, Mto Mara-Nitunze Nikutunze" ("I, Mara River-Stand with Me").*** Kaulimbiu hii imesheheni maudhui mazito yanayowataka wadau wote wa Bonde la Mto Mara kila mmoja kwa nafasi yake kuendelea kufanya shughuli ambazo ni rafiki kwa mazingira ya Bonde la Mto Mara. Aidha, Kaulimbiu hii inaweka mwelekeo wa kuendelea kushirikisha jamii katika maamuzi na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika Bonde hili.

**Ndugu Washiriki;** Nimeelezwa kuwa dhana ya kaulimbiu ya mwaka huu, inatekelezwa kwa vitendo na wilaya zote za Bonde la Mto Mara kwa upande wa Tanzania. Hii ni pamoja na uondoaji wa mifugo katika maeneo yasiyostahili ili kuzuia mmomonyoko wa udongo ambao hatimaye huharibu mazingira ya Bonde; upandaji

wa miti unaendelea kandokando ya kingo za Mto ndani ya eneo la mita 60 kama Sheria ya Mazingira ya Tanzania ya mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 zinavyoelekeza. Hizi ni juhudi kubwa zinazodhihirisha kwa vitendo utunzaji mazingira, rasilimali maji na hifadhi ya vyanzo vya maji.

## 3. HIFADHI YA MAZINGIRA NA VYANZO VYA MAJI

**Ndugu Washiriki,** Sote tunaelewa kwamba uhaba na uchafuzi wa vyanzo vya maji huathiri sekta nyingi, uhaba wa vyanzo vya Maji hutishia kutoweka kwa rasilimali maji na huhatarisha uhai wa viumbe vyote. Uchafuzi wa maji huhatarisha afya za viumbe hai ikiwemo mimea. Sekta zinazoathirika moja kwa moja na ukame ama uchafuzi wa maji ni pamoja na nishati, kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na viwanda. Kutokana na hali hiyo, na kwa kuzingatia umuhimu wa kutunza mazingira na vyanzo vya maji, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za

Maji namba 11 ya Mwaka 2009, pamoja na Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002. Sera ya Maji inasisitiza utunzaji shirikishi wa vyanzo vya maji. Aidha, Wizara pia inatekeleza Mkakati wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Mkakati huu unazungumzia masuala ya utunzaji, usimamizi na matumizi ya rasilimali maji nchini. Changamoto mbalimbali zimeainishwa katika Mkakati huu ambazo baadhi yake ni kama ifuatavyo:

i. Uharibifu wa mazingira utokanao na uvamizi wa wafugaji kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Nina furaha kuona kwamba hatua za kukabiliana na changamoto hii zinaendelea kuchukuliwa kwa kupunguza mifugo katika vijiji vyote vinavyozunguka Bonde la Mto Mara. Hii ni hatua nzuri ya utekelezaji wa Mkakati huu.

ii. Uharibifu wa mazingira unaotokana na uvamizi wa wakulima kwa ajili ya shughuli za kilimo kwenye miteremko

ya milima, mabonde na vyanzo vya maji. Pia nimejulishwa kuwa mkakati wa kuwaondoa wakulima kandokando ya vyanzo vya Maji unaendelea kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Maji pamoja na Wakurugenzi wa Wilaya zilizo kandokando ya Mto Mara. Ninasisitiza kwamba kazi hii inatakiwa kuwa endelevu kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kulinda mazingira ya Bonde la Mto mara kwa nchi zetu za Tanzania na Kenya.

iii. Uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni, mkaa na ujenzi wa nyumba mijini. Natambua ya kuwa hii ni changamoto kubwa kwa maisha ya wakaazi wote wa Bonde, kwani matumizi ya nishati mbadala ni muhimu. Kwa hili nimeambiwa kuwa jana tarehe 14 Septemba 2019 kulikuwa na semina mbalimbali zilizoelezea umuhimu wa hifadhi ya mazingira ya Bonde la Mto Mara ambapo maelezo ya athari za ukataji wa miti yalitolewa kwa kina. Ni

matumaini yangu kuwa hatua hiyo itasaidia kuongeza uelewa kwa wananchi kuona umuhimu wa kupanda miti ili kuhifadhi mazingira. Hivyo, zoezi la upandaji wa miti lililofanyika kandokando ya Mto litakuwa mwanzo mzuri kwa jamii kuendelea kupanda miti. Wito wangu kwa wananchi wote mnaoishi ndani ya Bonde la Mto Mara ni kuhakikisha kila kaya ina panda miti ya kutosha kwa mwaka ili kufidia kiasi cha miti kinachopotea kila siku. Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Wakuu wa Wilaya, pamoja na Wenyeviti wa Vijiji nchi nzima kuhamasisha upandaji miti rafiki kwa uhifadhi wa vyanzo vya maji na pia kuhakikisha miti iliyopandwa inatunzwa na kustawi.

iv. Umwagiliaji usiokuwa endelevu unaosababisha kutoweka kwa baioanuwai na upungufu wa maji ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme. Mahitaji ya umeme ni

muhimu sana katika masuala ya kiuchumi, hivyo upo umuhimu kwa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Mkoa wa Mara pamoja na Halmashauri zote kukaa pamoja ili kujadili kwa undani fursa zilizopo kuhusu eneo hili.

v. Uhaba wa kumbukumbu na takwimu sahihi kuhusiana na vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na maendeleo. Sote tunatambua kuwa bila takwimu sahihi maamuzi hayawezi kufanyika kwa usahihi. Uhifadhi wa kumbukumbu ni jambo la msingi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yeyote ile. Hivyo tuendeleze utaratibu wa kukusanya takwimu sahihi na tuwe na mfumo mzuri wa kuzihifadhi takwimu hizo.

vi. Uelewa na ushiriki mdogo wa wananchi katika hifadhi ya mazingira unadhoofisha jitihada za uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji. Kama nilivyozungumza hapo awali, mmechukua uamuzi mzuri wa kuendesha semina za utunzaji

wa mazingira katika Bonde la Mto Mara ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji katika maadhimisho haya ya Siku ya Mara. Hii itaongeza uelewa kwa wananchi hususan waishio kandokando ya vyanzo vya maji. Natoa wito kwa Wizara ya Maji pamoja na Mamlaka za Mkoa wa Mara kutekeleza miradi kwa kuzingatia kuwa wananchi wanashirikishwa kikamilifu ili kuhakikisha usalama endelevu wa miradi hiyo.

vii. Ukanda wa Bonde la Ziwa Victoria hususan Mkoa wa Mara una shughuli nyingi za uchimbaji madini. Hivyo, Baraza la Taifa la Mazingira, NEMC, pamoja na wadau wote tuhakikishe tunasimamia vyema Sheria ya Mazingira ya Namba 20 ya mwaka 2004 ili kuzuia uharibifu wa mazingira katika maeneo haya.

**Ndugu Washiriki,** Changamoto zilizoainishwa upande wa Tanzania hazitofautiani sana na zile ya Upande wa Kenya katika

kaunti za Bomet na Narok. Nachukua fursa hii kuomba washiriki wenzetu kutoka Kenya kuchukua hatua muafaka katika maeneo haya yote kwa kuwa uhifadhi na usimamizi wa Bonde la Mto Mara unategemea jitihada zinazochukuliwa kwa pamoja na kwa wakati mmoja kati ya Tanzania na Kenya.

**Ndugu Washiriki,** Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na Wenyeviti wa Vijiji kuwa mnao wajibu wa kulishughulikia kwa mtazamo chanya suala la utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji katika maeneo yenu kama ambavyo mnashughulikia masuala mengine. Suala la hifadhi ya mazingira ya Bonde la Mto Mara ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji limekuwa likitiliwa mkazo na Serikali ili kuhakikisha kuwa maji yaliyopo yanahifadhiwa na kutunzwa kwa mujibu wa sheria. Utunzaji wa mazingira ya Bonde la Mto Mara ni suala mtambuka ambalo linahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni

pamoja na sekta binafsi. Wito wangu kwenu ni kwamba tuendeleze ushirikiano katika uhifadhi wa mazingira ili pawepo na vyanzo vya maji vya uhakika, vyenye maji yakutosha na yenye ubora wakati wote kwa ajili ya maendeleo endelevu. Natoa wito kwa kila Halmashauri itilie mkazo suala la utunzaji wa mazingira ili kuwa na mazingira bora kwa usafi na afya na hatimaye kupunguza kuenea kwa magonjwa.

Katika kutekeleza suala hili, kila Halmashauri inapaswa kuendelea kuzingatia yafuatayo:

(i) kuongeza ufahamu na uelewa ndani ya jamii kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji;

(ii) kupanua ushirikishwaji wa jamii katika kuibua miradi mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji;

(iii) kuongeza uwajibikaji kwa watendaji na wadau mbalimbali katika suala zima la uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji.

## 4. HITIMISHO

**Ndugu Washiriki**, usimamizi madhubuti wa mazingira ya Bonde la Mto Mara na matumizi ya rasilimali maji katika sekta zote za kiuchumi na kijamii unahitajika ili kuleta tija kwa Taifa letu. Kwa upande wa Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Maafisa Maji wa Mabonde, mna wajibu wa kuhakikisha kuwa mnabuni mbinu na mikakati sahihi ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira ya vyanzo vya maji. Wadau wakubwa katika utunzaji wa vyanzo vya maji ni watumia maji na wananchi waishio katika mabonde ya maji, hivyo ni muhimu kuwaelimisha kuhusu kutumia maji kwa busara, uangalifu na kwa tija.

**Ndugu Washiriki**, ninatoa rai kwenu na kusisitiza kwamba tunawajibika kuongeza juhudi za pamoja kwa kushirikiana na

wenzetu kutoka Kenya kusimamia rasilimali maji za Bonde la Mto Mara kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**Ndugu Washiriki;** nahitimisha kwa kuwashukuru wote mliohudhuria maadhimisho haya ya Siku ya Mara. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania, ninawashukuru sana washiriki wenzetu kutoka Kenya na wahisani ambao kwa namna moja au nyingine mmewezesha shughuli hii. Aidha, nawashukuru wale wote mliohusika na maandalizi ya maadhimisho haya. Baada ya kusema hayo, naona fahari sasa kutamka kwamba Maadhimisho ya Siku ya Mara kwa mwaka 2019 sasa yamefungwa rasmi.

**‘Bila Uhifadhi na Usimamizi Imara wa Mazingira Bora ya Bonde la Mto Mara Hakuna Maendeleo’**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**